

Ibara za Imani

Aya ya 106 ya *Kitabu cha Mafundisho na Nidhamu*

¶ 106. IBARA ZA IMANI ZA KANISA LA METHODISTI ULIMWENGUNI.

Ibara za Imani hubaini viwango vya mafundisho vinavyopaswa kufuatwa na Kanisa la Methodisti Ulimwenguni. Kwa lengo hilo, huthibitisha desturi ya kanuni za imani za kanisa la ulimwengu, huonyesha urithi wetu wa imani wa kitheolojia wa Kiprotestanti, na hufafanua misisitizo na masuala mahususi ya imani ya Wesley na ya Kimethodisti ya kanisa letu. Ingawa Ibara za Imani hufafanua wajibu wetu kwa mafundisho sahihi ya Kikristo, tunatambua kwamba maneno ya asili ya Imani ya Nikea (mwaka wa 381 BK) yalisema kwamba Roho Mtakatifu hutoka kwa Baba, na kwamba makanisa mengi ulimwenguni na ndani ya Kanisa la Methodisti Ulimwenguni hayajakubali kauli ya nyongeza kuwa Roho hutoka pia kwa Mwana. Kwa kuakisi asili yake ya duniani nzima, waumini wa Kanisa la Methodisti Ulimwenguni tayari wana uhuru wa kujumuisha au kuacha maneno “na Mwana” wanapotumia Imani ya Nikea katika ibada na mafundisho ya imani (¶105). Kulingana na desturi hii kuhusu Imani ya Nikea, waumini wa Kanisa la Methodisti Ulimwenguni wanaweza kuacha maneno “na Mwana” katika sentensi ya kwanza ya Kifungu cha III, “Roho Mtakatifu.” Ibara za Imani huthibitishwa na Maandiko na zitafundishwa katika makanisa yetu. Ni viwango vya msingi vinavyotangaza “imani ambayo Mungu amewakabidhi watakatifu mara moja tu kwa wakati wote” (Yuda 3) na hutumiwa dhidi ya mafundisho ya uongo kwa kutoa msingi wa kumsifu na kumheshimu Mungu kupitia mafundisho ya uaminifu yanayotuelekeza kuishi maisha ya kutumikia ufalme wa Mungu.

I. UTATU MTAKATIFU

Tunaamini katika Mungu mmoja mtakatifu na aliye hai, wa milele, asiye na mwili wala sehemu, Muumba wa vitu vyote, vinavyoonekana na visivyonekana. Yeye hana kikomo katika nguvu, hekima, haki, wema na upendo, na anatawala huku akijali kwa neema ustawi na wokovu wa wote, kwa utukufu wa jina lake. Tunaamini kwamba Mungu mmoja anajidhihirisha jinsi alivyo: nafsi tatu zilizo tofauti lakini zisizotenganishwa, zilizo kitu kimoja daima katika asili, ukuu, uwezo na utukufu: Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

II. YESU KRISTO

Tunamwamini Yesu Kristo, Mungu wa kweli na mwanadamu wa kweli, Neno la milele lililofanyika mwili, ambaye ndani yake asili ya kimungu na ya kibinadamu zimeunganishwa kikamilifu bila kutenganishwa, bila kugawanywa, kuchanganya wala kubadilishwa. Kuhusu asili yake ya kimungu, yeye ni mmoja na ni kitu kimoja na Baba. Kuhusu asili yake ya kibinadamu, yeye ni mmoja na ni kitu kimoja na sisi, lakini hana dhambi. Mwana pekee wa Mungu aliyekuwepo tangu milele na Baba, akazaliwa na Bikira Maria kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Aliteseka kweli, akasulubiwa, akafa kwa ajili ya dhambi zetu, na akafufuliwa kimwili kutoka kwa wafu. Baada ya kupaa kwenye kiti cha enzi cha mbinguni, yeye ndiye Mwokozi na Mpatanishi wetu wa milele anayetawala juu ya vitu vyote na atarudi kwa utukufu kuwahukumu wazima na wafu.

Tunaamini Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake. Sadaka ya Kristo, iliyotolewa mara moja, ni kafara kamilifu, ukombozi, upatanisho, na fidia inayotosheleza kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote, dhambi ya asili na dhambi za mtu binafsi; wala hakuna fidia nyingine inayotosheleza kwa ajili ya dhambi.

III. ROHO MTAKATIFU

Tunaamini katika Roho Mtakatifu, anayetoka daima kutoka kwa Baba na Mwana. Yeye ni wa asili moja na Baba na Mwana na yuko sawa nao katika ukuu, uwezo, na utukufu. Kama Mungu wa milele na wa kweli, anastahili kuabudiwa na sifa zetu. Roho hufanya ulimwengu kutambua dhambi, haki na hukumu. Anamshuhudia Yesu Kristo, hutuelekeza kumwamini, hutujumuisha katika Kanisa, na hututakasa kupitia uwepo wake ndani yetu. Pamoja na Baba na Mwana, Roho Mtakatifu husambaza karama na kuliwezesha Kanisa kwa kila kitu kinachohitajika ili kutimiza lengo la Mungu duniani. Akiwa amana inayohakikisha utukufu

utakaokuja, anawafariji na kuwadumisha waaminifu na kutuongoza katika ukweli wote, akishuhudia pamoja na roho zetu kwamba sisi ni watoto wa Mungu.

IV. UUMBAJI NA UTUNZAJI

Tunaamini kwamba Mungu wa Utatu—Baba, Mwana na Roho Mtakatifu—aliumba vitu vyote pasipo kutumia kitu chochote, na hakuna kilichounda bila kuumbwa kwa mapenzi ya Mungu. Yote ambayo Mungu wa utatu anaumba ni mema, na aliviumba vitu vyote kama dhihirisho huru la upendo wake mkamilifu. Mungu huendelea kuhifadhi, kutawala na kudumisha viumbo wote kwa nguvu na hekima yake. Hiari na wajibu wa binadamu hufanya kazi katika muundo huu wa udumishaji.

V. ASILI YA BINADAMU

Tunaamini kwamba wanadamu waliumbwa kwa mfano na sura ya Mungu, na kwamba asili ya mwanadamu iliumbwa ikiwa nzuri na yenye heshima. Tuliumbwa kumpenda na kumtukuza Mungu katika wema wake mkamilifu, kuwapenda wengine, na kutamani na kufanya kazi kwa manufaa yao. Mungu alituumba wanaume na wanawake na alikusudia tuishi katika familia na jamii, na tuwe watumishi wa viumbe vyake vyema. Sasa tumeanguka katika uharibifu wa dhambi na tuko mbali sana na hali ya haki ya asili. Hata hivyo, bado sisi ni wa thamani isiyokadiriwa kwa Mungu.

VI. DHAMBI NA NEEMA YA BURE

Tunaamini kwamba wanadamu wameanguka kutoka kwenye haki ya asili na, mbali na neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, wanaendelea kufanya uovu tangu kuzaliwa. Dhambi ya asili, ambayo ni uharibifu wa asili ya kila mtu, ndiyo hali ambayo sote tumezaliwa ndani yake. Dhambi huharibu kila sehemu ya ubinadamu wetu. Mbali na neema tangulizi, hatuwezi kumgeukia Mungu na hatuwezi kufanya kazi zinazompendeza Mungu. Nia yoyote njema tulio nayo hutokana na neema ya Mungu katika Kristo na kazi ya Roho ndani yetu.

VII. KANISA

Tunaamini kwamba Kanisa linaloonekana ni ushirika wa waumini chini ya Uongozi wa Kristo. Kanisa ni moja, takatifu, la katoliki, na la kitume, katika asili na katika wito. Ni ushirika wa ukombozi ambapo Neno la Mungu huhubiriwa na sakramenti hutolewa ipasavyo kulingana na amri ya Kristo. Wanaume na wanawake waliohitimu huwekwa wakfu kwa ajili ya huduma katika Kanisa na maaskofu kwa kuwekelewa mikono. Chini ya nidhamu ya Roho Mtakatifu, Kanisa lipo kwa ajili ya kuabudu na kutukuza Utatu Mtakatifu, kuboresha tabia za waumini, na ukombozi wa ulimwengu.

VIII. MAANDIKO MATAKATIFU

Tunaamini katika uvuvio wa kimungu na mamlaka ya Agano la Kale na Agano Jipya, katika ukamilifu wake. Agano la Kale halipingani na Agano Jipya, kwani Kristo anatupa uzima wa milele katika yote mawili. Maandiko ni ya kweli katika kila jambo yanalolithibitisha, yanaaminika kabisa, na ndiyo sheria ya pekee isiyoweza kukosea katika imani na utendaji. Yana mambo yote yanayohitajika kwa wokovu. Chochote ambacho hakijafunuliwa katika Maandiko Matakatiifu au kuthibitishwa nayo hakipaswi kufundishwa kuwa ni muhimu kwa wokovu.

Roho Mtakatifu yuleyule aliyevuvia Maandiko anaendelea kufanya kazi kupitia Maandiko hayo, akiangazia jinsi Kanisa linavyoyafasiri kwa ajili ya kuboresha tabia za watu wa Mungu. Hayo ndiyo msingi wa mahubiri ya Kanisa na njia muhimu ya neema kwa wote wanaoyasikia. Kupitia kuhubiriwa kwa Neno, Roho hutufanya tutambue dhambi, hutuita kwenye toba, hutuvuta kwenye imani katika Kristo, na hutufanya upya katika mfano wa Mungu.

Vitabu rasmi vya Agano la Kale ni: Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, Kumbukumbu la Torati, Yoshua, Waamuzi, Ruthu, 1 Samweli, 2 Samweli, 1 Wafalme, 2 Wafalme, 1 Mambo ya Nyakati, 2 Mambo ya Nyakati, Ezra, Nehemia, Esta, Ayubu, Zaburi, Mithali, Mhubiri, Wimbo wa Sulemani, Isaya, Yeremia, Maombolezo, Ezekieli, Danieli, Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki, Sefania, Hagai, Zekaria, Malaki. Vitabu rasmi vya Agano Jipya ni: Mathayo, Marko, Luka, Yohana, Matendo, Warumi, 1 Wakorintho, 2 Wakorintho, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, 1 Wathesalonike, 2 Wathesalonike, 1 Timotheo, 2 Timotheo, Tito, Filemoni, Waebrania, Yakobo, 1 Petro, 2 Petro, 1 Yohana, 2 Yohana, 3 Yohana, Yuda, na Ufunuo.

IX. SAKRAMENTI

Tunaamini Sakramenti, zilizotawazwa na Kristo, ni ishara za nje na zinazoonekana za neema ya ndani na ya kiroho, na si tu ahadi au alama za ungamo la imani la Mkristo. Kwa hivyo, ni udhihirishaji wa upendo wa Mungu kwetu. Ni njia maalum ya neema ambayo Mungu hufanya kazi ndani yetu ili kuhuisha, kuimarisha, na kuthibitisha imani yetu kwake.

Tunaamini katika Sakramenti mbili tu ambazo zimetawazwa na Kristo Bwana wetu: Ubatizo na Meza ya Bwana.

Kuhusu Ubatizo

Tunaamini katika Ubatizo mmoja, unaoashiria kuingia katika Kanisa linaloonekana na Agano Jipya katika Kristo. Ubatizo ni ishara na muhuri wa kujumuishwa kwetu katika familia ya waumini katika muungano na kifo na ufufuo wa Kristo. Ubatizo unaashiria toba, kutakaswa kutoka kwa dhambi, na kuzaliwa upya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Tunaamini kwamba ahadi za Agano Jipya zinajumuisha watoto wa waumini, na hivyo watoto wachanga wanafaa na wanakubaliwa kubatizwa Kikristo, na hawapaswi kunyimwa ubatizo huo. Ni jukumu maalum la Kanisa kuwalea na kuwaongoza watoto waliobatizwa kwenye hakikisho la ubatizo wao kama ungamo la imani yao hadharani na kujitolea kwao binafsi kwa ufuasi wa maisha yote.

Kuhusu Meza ya Bwana

Tunaamini Meza ya Bwana ni Sakramenti ya ukombozi wetu ambapo tunafanywa washiriki katika matendo makuu ya wokovu ya Mungu. Ushirika Mtakatifu ni ukumbusho wa mateso na kifo cha Kristo na ishara ya upendo na muungano ambao Wakristo wanao na Kristo na kati yao. Ingawa vipengele vyenyewe havipaswi kuabudiwa, Roho Mtakatifu huwasilisha mwili na damu ya Kristo kwa namna ya fumbo kupitia Sakramenti kama njia ya neema, ingawa kiini cha kila kipengele hakibadiliki. Wale wanaopokea Sakramenti hii kwa unyenyekevu hushiriki kwa imani katika mwili na damu ya Kristo hadi atakaporudi.

X. IBADA YA HADHARA NA SIKU YA BWANA

Tunaamini kwamba ibada ya Mungu ni muhimu kwa maisha ya Kanisa, na ni wajibu na fursa ya pekee kwa Wakristo wote. Siku ya Bwana imeamriwa na Mungu kwa ajili ya ibada ya hadhara na ukumbusho wa ufufuo wa Kristo. Kukusanyika mara kwa mara kwa watu wa Mungu ni muhimu kwa ukuaji wa kiroho na utakaso wetu. Tunaamini utaratibu wa ibada ya hadhara unaweza kubadilishwa na kanisa kulingana na mahitaji ya jamii inayoabudu. Ibada inapaswa kufanyika daima kwa lugha na muundo unaoeleweka kwa watu waliokusanyika, kulingana na Maandiko Matakatifu na kwa mujibu wa utaratibu na nidhamu ya Kanisa.

XI. TOBA

Tunaamini kwamba Roho Mtakatifu anaufanya ulimwengu utambue hatia ya dhambi na anatuwezesha kuacha uovu na kuigeukia imani katika Kristo. Toba ya kweli hudhihirishwa kwa kuukana uovu na kuungama dhambi, na kwa kuanza kushiriki kikamilifu katika njia za neema na kujitahidi kutenda mema. Ni mtazamo wa unyenyekevu ambao Mungu huwapa wasioamini ili kuwatayarisha kwa kuhesabiwa haki, na huwapa waumini kama neema endelevu ambapo tunakua katika utakatifu na kuingia katika ushirika wa kina zaidi na Kristo.

XII. KUHESEBIWA HAKI NA KUZALIWA UPYA

Tunaamini kwamba kuhesabiwa haki ni tamko la Mungu alilolitoa kwa neema kwamba dhambi zetu zimesamehewa na kwamba tunahesabiwa kuwa wenye haki machoni pake kwa msingi wa ustahili wa Kristo. Tamko hili la Mungu linatujia kwa neema pekee kupitia imani pekee katika Yesu Kristo pekee. Kuhesabiwa haki si matokeo ya matendo yetu mema au ustahili wetu binafsi, kwani hakuna kinachoweza kutimiza matakwa ya haki ya Mungu isipokuwa dhabihu ya upatanisho ya Kristo msalabani, na hakuna kinachoweza kutusafisha kutokana na dhambi ya asili au dhambi tulizozitenda sisi wenyewe pasipo yeye. Kwa hivyo, tumealikwa kwa neema kumpokea Kristo kwa imani, tukiweka tumaini letu kamili kwake kama Bwana na Mwokozi wetu binafsi. Kupitia Kristo tunafanywa kuwa watoto wa Mungu na warithi wa uzima wa milele. Kufahamu kwamba tunahesabiwa haki kwa imani pekee ndilo fundisho kamilifu zaidi na faraja kuu.

Tunaamini kwamba kuzaliwa upya ni kufanywa upya kwa undani katika haki kupitia Yesu Kristo na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Tusipozaliwa upya, hatuwezi kuuona Ufalme wa Mungu. Kupitia kuzaliwa upya tunapatanishwa na Mungu, tunafanywa washiriki wa asili ya kimungu, tunapata hali ya maisha mapya katika Kristo, na tunawezeshwa kumtumikia kwa

upendo na hisia zetu. Kuzaliwa upya ni utakaso wetu wa awali, na baada yake tunafanywa upya hatua kwa hatua katika utakatifu tunapotafuta kukamilishwa katika upendo.

XIII. MATENDO MEMA

Tunaamini matendo mema ni matunda muhimu ya imani na hufuata kuzaliwa upya, lakini hayana uwezo wa kuondoa dhambi zetu au kuepusha hukumu ya Mungu. Tunaamini kwamba matendo mema yanayompendeza Mungu na yanayokubalika kwake katika Kristo hutokana na imani ya kweli iliyo hai. Kupitia na kwa matendo mema imani yetu inadhihirishwa. Hakuna matendo zaidi ya yale yaliyoamriwa katika Maandiko ambayo waumini wanaweza kutakiwa kuyatenda. Matendo yetu mema hayamlazimishi Mungu kutuonyesha fadhili, wala hayasababishi kustahili kwa wengine.

XIV. UTAKASO KAMILI

Tunaamini utakaso kamili ni hali ya upendo mkamilifu, haki, na utakatifu wa kweli. Ni kazi ya neema ya Mungu kupitia Neno na Roho. Utakaso kamili hupokelewa kupitia imani katika Kristo na unapaswa kutafutwa kwa bidii na kila mtoto wa Mungu. Wale waliozaliwa na Mungu tayari wamewekwa huru dhidi ya nguvu na utawala wa dhambi. Baadaye husafishwa dhidi ya dhambi ya asili na kuoshwa ili uchafu unaotokana nayo katika mawazo, maneno na matendo uondolewe. Waumini kama hao sasa wako huru kumpenda Mungu kwa mioyo yao yote, roho zao zote, akili zao zote na nguvu zao zote, na kuwapenda jirani zao kama wanavyojipenda wenyewe, wakifuata na kuzishika amri takatifu za Mungu.

Utaratibu wa utakaso huandaa njia ya kupokea neema inayotakasa kabisa, kupitia huduma ya Roho Mtakatifu. Tunaamini kwamba upendo mkamilifu, au ubora Wakristo, hautukomboi dhidi ya udhaifu, kutokujua au makosa yaliyo ya kawaida kwa watu wote, wala hauondoi uwezekano wa kufanya dhambi tena. Walio safi moyoni lazima wajilinde dhidi ya majaribu yanayoendelea, hasa yale yanayojitokeza kama kiburi cha kiroho, kwa kudumu katika utakatifu kupitia neema na uwezo wa Roho Mtakatifu.

XV. HUKUMU NA HALI YA BAADAYE

Tunaamini kwamba Kristo atarudi tena katika utukufu kuwahukumu wazima na wafu. Tunaamini katika ufufuo wa mwili: waovu watafufuliwa na kuhukumiwa adhabu ya milele, na wenye haki watafufuliwa na kupata uzima wa milele katika maumbo mapya ya Mungu.

Ilikubaliwa na Kongamano Kuu huko Johannesburg, Afrika Kusini, Jumamosi, tarehe 5 Septemba 2026.